WAZIRI wa Utamuduni na Jamii Bw. Kenneth Matiba akihutubia Wizara yake pamoja Waziri Mdogo wake Bw. Katana Ngala (katikati)
PICHA: KNA

BALOZI wa Oman Bw. Mohamed Musawi akipeana hundi ya Shs. 136,000 kwa Bw. Mohamed Amani wa Isahil Islamiyya kwa Mchango wa Lamu.
PICHA: KNA.

Madiwani Wawatumikie Wananchi Matatizo Yao

NINAPOANDIKA makala haya ni wazi kuwa Madiwani ambao watawatumikia wananchi katika Serkali za wilaya katika sehemu zao watakuwa wameshaanza kazi na kuona miji yetu inapiga hatua za kurishisha katika mambo muhimu yanayotuhusu yakiwa ya hali ya afya na elimu.

MHARIRI Wetu, *Abdulrahman Sheriff* **leo anatuzungumzia jinsi madiwani wanavyohitajika kuwahudumia wananchi waliowachagua katika uchaguzi mkuu uliofanika Septemba 26. mwaka huu.**

JAMBO muhimu zaidi ya yote ni kuona hali ya usafi wa miji yetu na hasa kwa wakati huu ambapo wananchi wanasumbuka mno kutokana na mbu wengi wanaowasumbua nyakati za kulala usiku; nyakati ambazo wananchi wanahitaji kulala bila ya kusumbuliwa ili asubuhi yake wapate kujishirikisha katika shughuli muhimu za kujitafutia riziki zao.

katika jiji la Mombasa pekeenazungumza juu ya jiji hili kwa sababu ndipo nilipo na yale yanayotokea ndio niyaonayo-hali ya usumbufu wa mbu yamezidi kupita nyakati zote zilizopita na wananchi wanawajibika wawe na dawa za kuchoma za mbu ama kama sivyo, basi ajue hatopata usingizi usiku kucha.

LAZIMA tukubali kwamba dawa hizi za mbu watu wengine kama wenye pumu, maradhi mengine, wazee na watoto haziwafai na huwafanya waugue zaidi ama wanapoinuka kukohoa kupita kiasi. Basi wengi kati ya hawa hukubali kuumwa na mbu kuliko kutaabishwa na moshi unaosambaa chumbani wa kufukuza mbu.

HALI kama hii ikibakia kwa muda mrefu, huenda wananchi wengi wakaugua kwa maradhi mabaya kama malaria na mengineyo. Ni juu ya madiwani wetu ambao wamechaguliwa hivi karibuni kufanya kila liwezekanalo kuona hali hii inamalizika mara moja.

KWA nini mbu wamezidi katika mitaa yetu? Hili ni swali ambalo kila mwananchi anajiuliza. Na jibu lake ni rahisi kwani mara nyingi mbu wanapatikana ikiwa mahli pana mizoga na uchafu. Kwa hivyo madiwani wetu hawana budi kupigana vita vya kuona hali ya usafi wa mji unapewa uzito wa hali ya juu.

MADIWANI wanawajibika kutembelea sehemu wananzoziwakilisha na kujionea wenyewe kwa macho yao kama hali ya uzoaji wa taka unaridhisha ama la! Kwani wakifanya hivyo ndipo watakapoweza kupeleka ripoti kwa wakuu wa idara inayoshughulikia jambo hili na hatua ya haraka kuchukuliwa.

WANANCHI wamewachagua madiwani kwa ajili ya kuwatumikia katika mambo kama haya na ni juu ya madiwani wenyewe kujua wajibu wao na kutoa huduma za utumishi wao kwa wananchi waliokubali kupigwa na jua ama mvua hata wakaitwa madiwani.

IKIWA madiwani watafanya ziara za kutembelea sehemu waziwakilishazo, basi sioni kama kuna shida yoyote ya uzoaji wa uchafu itakayotokea na ikiwa ni hivyo, basi nina uhakika mbu watapungua sana kama si kupotea kabisa.

KAMA Manispaa yetu ina dawa ya kufukuza mbu, basi kwa nini hawapiti mitaani na kutia dawa hizo badala ya kuacha wananchi kuteseka na mbu? Yataka ifahamike wengine wana uwezo wa kunua dawa za mbu kila siku na wengine hawana uwezo huo.

JAMBO jingine ambalo Manispaa yetu inahitaji kupigia darubini ni juu ya vichochoro ambavyo havimaliziki kwa matope na uchafu wa maji. Jambo hili pia husababisha kuchipuka kwa mbu wengi Ikiwa taratibu zitafuatwa, basi hapana shaka tatizo hili litamalizimka kabisa.

IKIWA Baraza letu litakuwa na fedha za kutosha, basi jambo jema la kufanya ni kujenga vichochoro hivyo kwa lami kama vile sehemu za Port Reitz zilvyofanywa. Barabara kama zilizoko sehemu hizo zataka pia zijengwe katika maeneo kama ya Majengo, Spaki, Mwembe Kuku na sehemu ambazo matope hayamaliziki hata kama hakuna mvua.

JUU ya Elimu, tatizo kubwa linalowakabili wazazi ni juu ya ukosefu wa watoto kupata darasa la kwanza kutokana na upungufu wa kuwa na madarasa. Jambo hili linawavunja nguvu sana wazazi ambao watoto wao wanakosa nafasi katika shule hizi za Manispaa.

HARAMBEE

NI juu ya madiwani kufanya taratibu za kuanzisha Harambee za majenzi zaidi ili watoto wetu wasikose nafasi ya masomo kwa ajili ya upungufu wa madarasa. Wazazi wako tayari kujishirkisha katika mikutano kama hii ambayo ni kwa manufaa ya masomo ya watoto wao.

NATARAJI makala haya yatawafikia madiwani wote waliochaguliwa na ingawa huenda kuna ya makosa niloyaandika, lakini yale ambayo ni ya manufaa kwa wananchi wote wa Mombasa, watayazingatia na kuyafuata sio kwa kuyafikiria pekee bali kwa vitendo!

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI
VYA FARUCCI KWA MSHINDI
WA KWANZA NA T-SHIRT
KWA WASHINDI WA PILI
NA WATATU KATIKA SHINDANO
JIPYA LA KUJAZA MANENO
SWAHILI CROSSWORD No. 172.



KWENDA KULIA:

1. Mlinzi wa mlangoni.
5. Histoa Mwanga na joto.
6. Sahibu, Mwandani.
8. Shahada ya elimu.
10. Mfuko wa Ngozi pengine hutiwa maji kama mtungi.
12. Shikamana.
15. Umoja wa mataifa
16. Namna ya samaki wa bahari
18. Akuweke nje.
19. Kinyume cha "Ni".

KWENDA CHINI:

1. Neema
2. Kulia kwa risasi katika bunduki.
3. Malipo ya mfanyi kazi wa kibarua.
4. ..... hukatikia pabovu.
7. Zamani, wakati uliyopita.
9. Tamko la kukataa.
11. Nchi huru katika Asia.
13. Chumvi.
14. Mahindi ya kukaangwa.
17. Boma kando ya nyumba.

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 171.

1. Simeon Tawa, Sanduku La Posta 81504, MOMBAA.

2. Habibu Omari, Sanduku la Posta 81211, MOMBASA.

3. Bi Pauline S. Owambo, Sanduku La Posta 73, MARIAKANI.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANANO No. 171.

KWENDA KULIA

3. DO, 4. KARAKANA, 6. DM, 7. KOKO, 9. TAI, 10. WA, 11. CHANGENI, 13. MA, 14. DA, 15. APA, 16. UK.

KWENDA CHINI

1. FAA, 2. IDADI, 5. RUKWAMA, 7. KUCHA, 8. OANA, 12. IDI.

JINA..

SANDUKU LA POSTA..........................

....

Shindano la Fumbo La Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwe Muhariri COASTWEEK Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya Siku ya jumatono tarehe **Oct. 26 1983**, saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho

ZIKENI TOFAUTI . . .

ALIEKUWA Mjumbe wa Coast Advisory Council, na Mwenyekiti wa Idara ya Afya katika Jimbo la Pwani, Bwana Abubakar Yusuf Gandy, amewataka madiwani wa Mji wa Mombasa, wasahau tafauti zao za kisiasa na kushirikiana kama kundi moja kwa amani.

Bwana Gandy amewashauri madiwani walio chaguliwa uchaguzi huu wa Nyayo kufuata mawaidha ya Mtukufu Rais Moi, kongozi mwenye hekima na busara anae taka wakati wa uchaguzi, wanainchi wawachague viongozi wenye moyo

KAZI

wa kuwatumikia wanainchi na wenye ujuzi na kuzielewa kazi hizo watakazopewa.

Itakuwa ni vizuri viti na wenye ujuzi na kuzijua kazi zao, ili mji wa Mombasa upate maendeleo zaidi na itakuwa vibaya mukiwachgua viongozi wasiokuwa na ujuzi wowote katika baraza la Mji. Itakuwa ni kama kusimamisha maendeleo ya Mji wa Mombasa - yasiendelee.

MOI

Kwa hishima kubwa anapmongeza mtukufu Rais Moi, kwa kutawazwa tena kwa mara ya tatu kama Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Kenya na Rais wa Jamhuri ya Kenya.

"Mungu ampe maisha marefu na afya njema azidi kuongoza taifa letu, kwa filosofa ya enzi ya NYAO, AMANI, UPENDO na UMOJA. Mungu Atusaidiye, Alisema Bw. Gandy.

MWANA KHAMIS

MREMBO Anastasia Khamis anayefanya kazi mjini Mombasa. Yeye ni Mzaliwa wa Mkoa wa Nairobi, na ana umri wa miaka (18). Anapendelea kwenda Cinema, kuogelea, kusoma Biblia na ***Coastweek*** **kila siku ya Ijumaa.**

PICHA: CAESAR MADDANGANHA.